Jina _____ Nambari _____

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA I
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011
SAA: 1 ¾

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1
SAA: 1 ¾

MAAGIZO

1. Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
2. Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo tatu zilizobakia.
3. Kila insha isipungue maneno 400.
4. Kila insha ina alama 20.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

MASWALI

1. Wewe ni Mwanahabari katika shirika la KTV. Andika mahojiano kati yako na waziri wa kilimo nchini kuhusu athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabiliana na tatizo hili

2. Usione tanga la njaa ukasahau la miyaa.

3. Serikali imeunda hazina ya vijana ambayo lengo lake ni kuvipa vikundi vya vijana misaada ya kifedha ili wajiajiri katika miradi kabambe, Pendekeza jinsi wewe na kundi lako mtatumia msaada huo mkipewa.

4. Andika insha itakayomalizia kwa
…….. Moshi ulifurika anga nzima kumbe unyama umewatoka wanyama na kuwaingia watu.

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA I
INSHA
JULAI / AGOSTI 2011

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 1

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. SWALI LA KWANZ A
MAHOJIANO
Athari za baa la njaa

1. Vifo vya binadamu au watu.
2. Vifo vya mifugo.
3. Shule hufungwa kutokana na ukosefu wa chakula.
4. Maradhi mbalimbali yanazuka mf utapiamlo.
5. Kuhama kwa jamii kutafuta chakula.
6. Pato kubwa la kitaifa hutumika kushughulikia njaa
7. Kudumaa kwa maendeleo ya wananchi na taifa.
8. Wanasiasa au matajiri hujinufaisha wakitumia fursa hii.

HATUA ZINAZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA BAA LA NJAA

1. Serikali kutangaza baa la njaa kama janga la kitaifa.
2. Kibuni kwa wizara inayoshughulikia tatizo hili.
3. Misaada ya chakula kwa wahasiriwa kutoka kwa serikali na wahisani wengine.
4. Serikali inunue mifugo kutoka kwa wakulima walioathiriwa na njaa.
5. Wakulima wahimizwe kupanda mimea inayoweza kuhimili ukame.
6. Wakulima wapewe mbegu za kupanda zinazochukua muda mfupi kukomaa.
7. Serikali inajenga mabawa ya kukusanya maji wakati wa mvua na kuyahifadhi
8. Serikali itenge mamilioni ya pesa ya kuimarisha shirika la nafaka nchini NCPB na kununua pamoja na kuhifadhi mazao.

TANBIHI
1. Mtahiniwa azingatie sehemu mbili za mahojiano.
2. Athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali pia zizingatiwe. Asipozingatia sehemu zote mbili atolewe alama (4m)
3. Sura ya mahojiano ichukue mtindo wa tamthilia unaohusisha maswali na majibu
4. Majina ya mhojiwa na mhoji au vyeo vyao yaandikwe
5. Asipozingatia sura atolewe alama (4s)
6. Asipozingatia urefu unaotakikana wa maneno kati ya 375- 400 aondolewe alama (2u)
7. Mwanafunzi ajihusishe kama mhusika. Asipojihusisha aondolewe alama. (2)

Kijitabu hiki kina kurasa 7 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

2 SWALI LA PILI
METHALI
Usione tanga la nguo ukasahau la mijaa
Maana na matumizi ni kama yale ya:

(i) Usiache mbachao kwa mswala upitao
(ii) Usisahau ubaharia kwa sababu ya unahodha.

Mwanafunzi atunge kisa kinachoonyesha maana kuwa usimwache rafiki yako wa siku zote kwa kumpata rafiki mpya. Hii ni kwa sababu kuwa yule mpya huenda akakuacha ukamtamani yule rafiki wa zamani na pengine usimpate.

3. SWALI LA TATU
Jinsi kundi litatumia msaada kutoka kwa hazina ya vijana.

Mwanafunzi alenge yafuatayo:
(a) Tatizo ambalo mradi wao unalenga kutatua – ataje mradi wenyewe mf ufugaji wa kuku.
(b) Mwanfunzi aeleze lengo / madhumuni ya mradi
(c) Njia zitakazofuatwa ili kutekeleza madhumuni ya mradi.
(d) Ataje vifaa vitakavyohitajika
(e) Ataje makadirio ya gharama ya mradi.
(f) Njia za kuhudumisha mradi huu pia zitajwe

4. SWALI LA NNE
Dhana ya watu kutendea watu wengine vitendo vya kinyama ijitokeze mf kuwaua watu wengine, kuwanajisi, kuwaibia mali yao, kiwachomea nyumba / mali n.k

TANBIHI
1. Mwanafunzi anapoanzisha insha kwa maneno / mdokezo uliopeanwa atakuwa amejitungia swali hivyo awekwe kiwango cha D ya chini.
2. Akiyapunguza au kuyaongeza maneno katika mdokezo, aondolewe alama (4m)

HITIMISHO

MWONGOZO W KUSAHIHISHA INSHA

USAHIHISHAJI
Karatasi hii imedhamiria kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi, zenye utiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia. Ubunifu mwingi na hali nadhifu. Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini lazima asome insha ili aweze kuikadiria akizingatia viwango mbalimbali vilivyopendekezwa, yaani A, B, C na D, kutegemea kiwango chochote kile kinachostahili.

KIWANGO CHA D
MAKI 01 – 05

1. Insha ya aina hii haieleweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa
3. Lugha imevurugika, uakifishaji haufai, na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi, kimaendelezo, kimtindo n.k.

VIWANGO TOFAUTI VYA 'D'
D- (KIWANGO CHA CHINI) Maki 01 -02

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile. Kwa mfano kunakili swali au kujitungia swali tofauti na kulijibu.
2. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi
3. Anayenakili kichwa tu; anayenakili kichwa na kukikariri
4. Anayenakili maswali yote na kuyakariri.
5. Anayejitungia swali lake na kulijibu

D (WASTANI) Maki 03
1. Insha haieleweki
2. Utiririko wa mawazo haupo
3. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukuzwa vilivyo
4. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui
5. Matumizi yake ya lugha ni hafifu mno
6. Kuna makosa mengi ya kila aina.

D+ (KIWANGO CHA JUU) Maki 04-05
1. Insha hii ina makosa mengi ya kila aina, lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Insha ina lugha dhaifu ya Kiswahili na haina mpangilio
3. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka kikamilifu
4. Hana uhakika wa matumizi ya lugha na hupotoka hapa na pale
5. Mtahiniwa hujirudiarudia
6. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza, k.m 'papa' badala ya 'baba' karamu badala ya 'kalamu' n.k
   Insha – asipoonyesha ni hafla ya kuchangisha pesa

KIWANGO CHA 'C'
MAKI 06 – 10

Kiwango hiki kina makosa yafuatayo:
1. Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia mada, japo mada haikukuzwa na kuendelezwa vilivyo.
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia
3. Hana ubunifu wa kutosha
4. Anaakifisha sentensi vibaya
5. Hana msamiati wa kuvutia wala msamiati mwafaka
6. Kuna makosa mengi ya sarufi, msamiati na hijai (tahajia)

VIWANGO TOFAUTI VYA C

C – (KIWANGO CHA CHINI) MAKI 06-07

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake
2. Mada haijakuzwa na kuendelezwa kwa njia ifaayo
3. Hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo
4. Ana makosa mengi ya sarufi, tahajia na msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.

C (WASTANI) Maki 08

1. Anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu
2. Dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi
3. Hana ubunifu wa kutosha
4. Utiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa
5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa
6. Uafikishaji wa sentensi zake si mzuri
7. Ana makosa mengi ya sarufi, hijai na msamiati lakini bado insha inaeleweka.

C+ (KIWANGO CHA JUU) Maki 09-10

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada, lakini kwa njia isiyo na mvuto.
2. Dhana tofauti tofauti zimeanza kujitokeza japo kwa njia hafifu
3. Kuna utiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa
4. Misemo, methali na tanakali za sauti zimetumiwa kwa njia hafifu
5. Uakifishaji wake si mzuri.
6. Kuna makosa ya sarufi, msamiati na hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo

KIWANGO CHA 'B'

Maki 11 – 15

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha kiumudu lugha vilivyo
2. Mtahiniwa anadhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza.
3. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri
4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha kama vile kuandika sentensi kwa njia tofauti tofauti na zikaleta maana ile aliyokusudia.
5. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.

VIWANGO TOFAUTI VYA B

B- (KIWANGO CHA CHINI) Maki 11 – 12

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake vizuri akieleza hoja tofauti tofauti akizingatia mada
2. Ana utiririko mzuri wa mawazo
3. Anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia
4. Sarufi yake ni nzuri
5. Makosa yanadhihirika

B (WASTANI) Maki 13

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha
2. Mawazo yake yanadhihirika akizingatia mada
3. Anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka
4. Sarufi yake ni nzuri
5. Kuna makosa machache

B+ (KIWANGO CHA JUU) Maki 14-15
1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi, akizingatia mada.
3. Uteuzi wake was msamiati ni mzuri / ana mchanganyiko wa msamiati
4. Sarufi yake ni nzuri
5. Uakifishaji wake ni mzuri
6. Makosa ni machache ya hapa na pale

KIWANGO CHA 'A'
Maki 16 – 20
1. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato. Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka.
2.Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi
3. Umbuji wake unadhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na wa hali ya kumvutia msomaji wake.
4. Kazi yake ni nadhifu na hati yake ni nzuri.

A- (KIWANGO CHA CHINI) Maki 16-17
1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha
2. Mawazo yanadhihirika na anaishughulikia mada
3. Ana utiriko mzuri wa mawazo
4. Msamiati wake ni wa kuvutia
5. Sarufi yake ni nzuri
6. Anatumia miundo tofauti ya sentensi vizuri
7. Makosa ni machache yasiyokusudiwa

A (WASTANI) Maki 18
1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kulingana na mada
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato
3. Anatoa hoja zilizokomaa
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri
6. Makosa ni nadra kupatikana

A+ (KIWANGO CHA JUU) Maki 19-20
1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughulikiwa vilivyo
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato
3. Hoja zake zimekomaa na zinazoshawishi
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unaovutia zaidi
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kwa ufundi.
7. Jumla ya makosa yake isizidi matano. Idadi ya makosa yake isizidi matano

KIWANGO	ALAMA	MAKI
A	A+ A A-	19 – 20 18 16 – 17
B	B+ B B-	14 – 15 13 11 – 12
C	C+ C C-	09 – 10 08 06 – 07
D	D+ D D-	04 – 05 03 00 – 02

JINSI YA KUTUZA INSHA MBALI MBALI

1. Mtahiniwa asipozingatia sura ya insha aondolewe maki 4 (nne) baada ya kutuzwa (4 sura)
2. Insha isiyotosheleza idadi ya maneno itaondolewa maki 2 (mbili) baada ya kutuzwa (2u)

SARUFI

Sahihisha kwa makini sana ukionyesha makosa yote yanayotokea. Makosa ya sarufi huwaratika.

1. Kuakifisha vibaya. Kwa mfano, vikomo, vituo, alama ya kuulizia n.k
2. Kutumia herufi ndogo au kubwa mahali si pake
3. Matumizi mabaya ya ngeli na viambishi, nyakati, vihusiano, muundo mbaya wa sentensi na mnyambuliko wa vitenzi na majina.
4. Kuacha au kuongeza neno katika sentensi, kwa mfano, 'Kwa kwa"
5. Matumizi ya herufi kubwa.

    (a) Mwanzo wa sentensi
    (b) Majina ya pekee
        i. Majina ya mahali, miji , nchi
        ii. Siku za juma, miezi n.k
        iii. Mashirika, masomo, vitabu n.k.
        iv. Makabila, lugha n.k
        v. Jina la Mungu
        vi. Majina ya kutambulisha k.m. Majina ya mbwa k.v Tom, Jim, Peter

MAKOSA YA HIJAI / TAHAJIA

Haya ni makosa ya maendelezo . Sahihisha ukiyaonyesha yanapotokea. Makosa ya tahajia huwa katika:-

1. Kutenganisha neno kama vile 'aliye kuwa'
2. Kuunganisha maneno kama vile 'kwasababu'
3. Kukata silabi vibaya kama vile 'ngan-o'
4. Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama 'mahari' badala ya 'mahali'
5. Kuacha herufi katika neno kama 'aliekuja' badala ya 'aliyekuja'
6. Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama 'piya' badala ya 'pia'
7. Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika herufi. k.m j,I – kitone.
8 Kutoandika kistari cha kuunganisha neno ufikiapo pambizo, au mwisho, au kuandika mahali si pake.
9. Kuacha ritifaa au kuiweka pasipofaa. Ngombe, ngom'be, n'gombe
10. Kuandika maneno, kwa kifupi mfano, k.m, n.k, v.v

MTINDO

Mambo yatakayochunguzwa

1. Mpangilio wa kazi kiaya
2. Utiririko wa mawazo
3. Hati nzuri inayosomeka kwa urahisi
4. Namna anavyotumia tamathali za usemi k.m methali, misemo, jazanda n.k
5. Kuandika herufi vizuri, k.m, Jj, Pp, Uu n.k
6. Sura ya insha
7. Kujiridhisha

MSAMIATI

Jumla ya maneno yaliyotumiwa kuafikiana na mada au kichwa kilichopendekezwa

MAUDHUI NA MSAMIATI

Baada ya kusoma mtungo utafikiria maudhui na msamiati uliomo kwa jumla

ALAMA ZA KUSAHIHISHIA

= Hupigwa chini ya sehemu ambayo kosa la sarufi limetokeza kwa mara ya kwanza

__ Hupigwa chini ya sentensi au neno ambako kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

^ Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno

√ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe
Maelezo mafupi kuhusu tuzo la mtahini yanahitajika. Kila ukurasa uwe na alama ya √ chini katikati kuonyesha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati. Alama hii hutiwa juu ya neon lenyewe

MANENO

Maneno	8	-	ukurasa 1 ¾
Maneno	7	-	kurasa 2
Maneno	6	-	kurasa 2 ¼
Maneno	5	-	kurasa 2 ¾
Maneno	4	-	kurasa 3 ¾
Maneno	3	-	kurasa 4 ½

Neno	1 – 174	-	Robo
	175 – 274	-	Nusu
	275 – 374	-	Robo tatu
	375 – 400	-	Kamili

Jina _____ Nambari _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011
SAA: 2 ½

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2
SAA: 2 ½

MAAGIZO

Jibu maswali yote katika nafasi zilizoachwa.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Kijitabu hiki kina kurasa 10 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukuraza

UFAHAMU

Kushamiri kwa wimbi la uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii na hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri upo ushahidi kuonyesha kuwa wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, watu wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia . Matokeo yake ni mengi. Haya ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binaadamu hunata zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu, vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyafanya sehemu ya masiha yao. Wengi huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji. Kuna wale ambao huanza kujichua. Kujichua ni hali ya mwanamke au mwanaume kumaliza haja za kimaumbile bila kufanya mapenzi na mtu mwingine. Ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya

Jambo hili limegeuza mielekeo ya vijana kwani wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila kuchapo.

Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji wa pombe, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana tabia za unyama.

Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani kuondoa makali. Hata katika utu nzima, mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kukinga jamii kutokana na maenezi haya yasiyo na kizuizi. Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Kwa namna hili litawezekana kupunguza mahitaji na uuzaji wa ponografia. Aidha ni vizuri watu wazima wawajibike ili wawalinde hasa vijana kutokana na athari hizi. Inapasa wenye midahilishi, video na sinema wasiwaruhusu vijana kutazama uchafu huu.

Tatizo la kuenea kwa ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sheria. Kilichoko basi ni kuweka sheria za kuzuia utengenezaji na usambazaji wa upujufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mzima. Serikali na mashirika ya midahilishi yajumhike kutambua chanzo cha taka hizi kisha wanaohusika wakabiliwe ipasavyo. Jamii ingependa kuona michakato ya kuharamisha, usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wasaidie. Ni muhimu washikilie kwa dhati juhudi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia uongofu na kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa kiafrika unakataza vikali mtu kuona uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu wa jamii.

1. Ufahamu

(a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 1)

_____

_____

_____

(b) Kina nani hushawishika zaidi na wimbi linalozungumziwa katika taarifa na huathirika vipi? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(c) “Vijana wengi ni kama bendera.” Fafanua huku ukitoa mifano kutoka kwenye taarifa uliyosoma. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(d) Taja athari za kudumu zinzosababishwa na utazamaji wa ponografia. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(e) Kutokana na taarifa jamii inaweza kujikinga na mabaya ya ponografia vipi? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(f) Serikali yafaa kuchukua hatua gani kupigana na uovu huo katika jamii? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

_____

(g) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 2)

(i) Ponografia

_____

_____

_____

(ii) Najisi

_____

_____

_____

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza, ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa kutoka kizazi kimoja kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitaji mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitaminiB vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini) bidhaa za soya, matunda, maziwa, bidhaa za ngano, samaki pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madini haya ni mboga za kijani, dengu, mawele, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati, awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini kwa hivyo vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisichohatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni mujimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kuvuruga akili. Vurungu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na namna ya kukitoa.

Hali kadhalika mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na ratiba ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya haya mazoezi ya kiakili kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo na vitanzandimi, ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

2. Ufupisho

(a) Eleza mchango wa chakula katika huimarishaji wa uwezo wa kukumbuka (Maneno 60 – 65) (alama 5)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 70-80 (alama 7)

Matayarisho

Nakala safi

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

3. Matumizi ya lugha

(a) Taja konsonati mbili ambazo hujulikana kama nusu irabu. (alama 2)

_____

_____

_____

(b) Nomino hizi ziko katika ngeli gani?

(i) Sukari _____

(ii) Nyangumi _____ (alama 2)

(c) Kamilisha sentensi hii kwa neno lililo kinyume na lililopigiwa mstari.

(i) Maji <u>yameganda</u> huwezi _____ (alama 1)

(d) Tenganisha mofimu katika maneno yafuatayo.

(i) Mgonjwa

_____

_____

_____

(ii) Sungura (alama 2)

_____

_____

_____

(e) Andika sentensi hii katika umoja.

(i) Nyavu za akina mama hazishiki nguva. (alama 2)

_____

_____

_____

(f) Andika sentensi mbili ukitumia neno shujaa kama

(i) Kivumishi

_____

_____

_____

(ii) Jina (alama 2)

_____

_____

_____

(g) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.

(i) Wapatie nafasi wanakandarasi wale. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(h) Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi .

(i) Aidha

_____

_____

_____

(ii) Sembuse (alama 2)

_____

_____

_____

(i) Sentensi hizi ni za aina gani?

(i) Chakula kingi kilipikwa lakini hakikutosha

_____

_____

_____

(ii) Mwalimu mkuu alipofika shuleni wanafunzi wote walikuwa wameshaondoka. (alama 2)

_____

_____

_____

(j) Pigia nomino mistari na ueleze ni za aina gani.

(i) Kuimba kwa Bwana Zohari hunipa raha. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(k) Tunga sentensi kubainisha tofauti iliyoko kati ya:

(i) Kacha

(ii) Kasha (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(l) Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo.

Nafsi ya tatu umoja

Wakati uliopita

Kirejeshi

Kitendwa

Mzizi

Kiishio (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(m) Andika sentensi hii katika usemi halisi

Mjomba alisema angesafiri kwenda Dubai alasiri hiyo. (alama 3)

_____

_____

_____

(n) Tunga sentensi ili kuonyesha matumizi ya ‘Kwa’ katika maana ya

(i) Ala kitumizi

_____

_____

_____

(ii) Pamoja na (alama 2)

_____

_____

_____

(o) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

(i) Vitabu vichafu vimeuzwa leo

_____

_____

_____

(ii) Amepanga chumba chenye mwanga hafifu. (alama 2)

_____

_____

_____

(p) Andika vitenzi hivi katika hali ya kutendesha.

(i) Nawa

_____

_____

_____

(ii) Takata (alama 2)

_____

_____

_____

(q) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha vitenzi vilivyopigiwa mistari kuwa nomino .

(i) Yeye hufuma mikeka vizuri na kuwavutia wengi. (alama 2)

_____

_____

_____

(r) Tumia neno ‘hadi’ kama kihuzishi cha

(i) Kiwango

_____

_____

_____

(ii) Wakati

_____

_____

_____

(iii) Mahali (alama 3)

_____

_____

_____

(s) Kiakifishi hiki ’ huitwaje (alama 1)

_____

_____

4. Isimu Jamii

Tom: Vipi Tracey! Naona leo unalinga sana. Umenivaria miwani, mbona hivi? Is it because you are very smart today?

Tracey: Niko poa! Hata hivyo naona una yako mengine wewe! Siringi, Nikobusy tu sana. Plus company yako inatisha, hujui siku hizi nimechill. Tena umenibore.

Tom: Kumbe wewe ni ……..

(a) Taja sajili inayojitokeza katika dondoo hii. (alama1)

_____

_____

_____

(b) Taja mifano inayojitokeza katika dondoo ya :

(i) Kubadili msimbo

_____

_____

_____

(ii) Kuchanganya msimbo (alama 2)

_____

_____

_____

(c) Ni kwa nini wazungumzaji hubadili na kuchanganya msimbo. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(d) Ni mzungumzaji yupi ana lafudhi? Ni nini maana ya lafudhi? (alama 2)

_____

_____

(e) Taja sababu mbili za kuwa na lafudhi.

_____

_____

_____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. UFAHAMU

(a) Ponografia / Athari za ponografia n.k (alama 1)

(b) Vijana hushawishika zaidi. Huathiri / huharibu akili au hisia na badala ya kuzingatia masomo huzingatia mambo machafu. (alama 2)

(c) Vijana huiga wanayoyaona na kusikia k.m
(i) Hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema.
(ii) Kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao.
(iii) Kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji.
(iv) Huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono.
(alama 4 x 1 = 4)

(d) Kupoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtazamaji wa ponografia. (alama2)

(e) (i) Kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi.
(ii) Watu wazima wawajibike ili walinde vijana kutokana na athari hizi.
(iii) Wenye midahilishi, video na sinema wasiwaruhusu vijana kutazama uchafu huu.
(Zozote 2 x 1 = 2)

(f) (i) Kuweka sheria za kuzuia utengenezaji na usambazaji wa upungufu huu
(ii) Hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi
(iii) Serikali na mashirika ya midahilishi yajumhike kutambua chanzo cha taka hizi kisha wanaohusika wakabiliwe ipasavyo
(Zozote 2 x 1 = 2)

(g) (i) Picha / filamu za watu walio uchi (alama 2)
(ii) Uchafu / chafu

Makosa sarufi hadi ½ x 10 = 5
Hijai hadi ½ x 6 = 3

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

2. UFUPISHO

(a) 1. Vyakula vinavyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia uwezo wa kukumbuka.

2. Vyenye madini ya chuma huwecha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi.

3. Glukosi inayopatikana kwenye vyakula vyenye sukari ni muhimu kwa ubongo nyakati zote.

4. Vyenye nyuzinyuzi huhakikisha mwili una kiwango cha sukari kisichohatarisha mwili

5. Vileo na nikotini huzorotesha uwezo wa kukumbuka

Hoja 5 x 1 = 5

(b) 1. Woga na kivurugika akili ni mambo tunayopaswa kuepuka kila wakati.

2. Ni kawaida mtu kukabiliwa na woga anapopatana na jambo asilokuwa na hakika na matokeo yake.

3. Umpatapo awe makini usimvuruge akili.

4. Mwili wenye siha nzuri huhakikisha ubongo ni timamu.

5. Mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na kuimarisha uwezo wa kukumbuka mambo.

6. Ratiba ya kunyoosha viungo ni muhimu

7. Mazoezi ya kiakili hustawisha uwezo wa kukumbuka.

8. Uimarishaji wa uwezo huu ni muhimu kimaendeleo na unahitaji mchango wa kila mwana-jamii.

Hoja zozote 7 x 1 = 7

Makosa Sarufi hadi ½ x 10 = 5
Hijai hadi ½ x 6 = 3
Utiririko alama 3

3. Matumizi ya Lugha

(a) Nusu irabu /w / / y / (2 x 1 = 2)

(b) Sukari i – i
Nyangumi A – wa 1 x 1 = 1

(c) Kuyayeyusha 1 x 1 = 1

(d) (i) M – gonjwa
(ii) Sungura (mofimu huru) 2 x 1 = 2

(e) Wafu wa mama hauishiki nguva. (alama 2)

(f) Km Kijana shujaa ametuzwa (kivumishi) 1 x 1 = 1
Shujaa amekwenda vitani (Nomino) 1x 1 = 1

(g) Wale – kiashiria 1 x 1 = 1
Wale – Kupata chakula (kutia chakula kinywani) 1 x 1 = 1

(h) (i) Aidha : Vile vile, pia, isitoshe, kadhalika
(ii) Sembuse: Hutumiwa kuonyesha kinyume hasa pale ambapo pana ulinganishi wa watu wawili au vitu viwili, kimoja cha hadhi na kingine kisichokuwa cha hadhi. 2 x 1 = 2

(i) (i) Sentensi ambatano 1 x 1 = 1
Sentensi changamano 1 x 1 = 1

(j) Kuimba – kitenzi jina
Bwana Zohari – Nomino ya kipekee
Raha – Nomino ya dhahania (alama 3)
Kutambua alama ½
Kutaja alama ½

(k) Kacha – Ng'ang'ania / shikilia jambo bila ya kukubali jingine. 1 x 1 = 1
Kasha – Sanduku kubwa liwekwalo vitu vya thamani. 1 x 1 = 1

(l)

Km	Nafsi ya tatu	–	a	alama ½
	Wakati uliopita	-	li	alama ½
	Kirejeshi	-	ye	alama ½
	Kitendwa	–	m	alama ½
	Mzizi	–	pig	alama ½
	Kiishio	-	a	alama ½
				3

(m) " Nitasafiri kwenda Dubai leo alasiri." Mjomba alisema. Alama 3

(n) Kitumizi km Alimpiga kwa fimbo. 1 x 1 = 1
Pamoja na km Walifika mkutanoni wake kwa waume. 1 x 1 = 1

(o) (i) Kirai nomino 1 x 1 = 1
(ii) Kirai kivumishi 1 x 1 = 1

(p) Nawa – Navya 1 x 1 = 1
Takata – Takasa 1 x 1 = 1

(q) Ufumaji wake wa mikeka huwa na mvuto kwa wengi. (alama 2)

(r) Mfano (i) Maji yamejaa hadi pomoni . 1 x 1 = 1
(ii) Walicheza hadi jioni. 1 x 1 = 1
(iii) Walimkimbiza hadi kwake nyumbani. 1 x 1 = 1

(s) Ritifaa 1 x 1 = 1

4. Isimu Jamii

(a) Sajili ya vijana 1 x 1

(b) (i) Kubadili msimbo – Or is it because you are very smart today.
(ii) Kuchanganya msimbo. Nikobusy, Umenibore, nimechill. 2 x 1

(c) (i) Kwa sababu ya kuwa na umilisi wa lugha mbili au zaidi.
(ii) Kwa sababu ya kukosa msamiati mwafaka wa kutumia katika lugha moja.
(iii) Ili kujinasibisha na kundi moja la watu.
(iv) Ili kuonyesha kuwa unaifahamu lugha hasa iliyo na hadhi fulani katika jamii.
(v) Ili kuificha maana kutoka kundi moja la watu. 3 x 1

(d) Tom: √1
Lafudhi ni namna mtu anavyoyatamka maneno yake. √1

(e) (i) Kwa sababu za athari ya lugha ya mama.
(ii) Kwa sababu za athari ya lugha zingine zinazomzunguka mzungumzaji.
(iii) Kwa sababu ya kasoro fulani iliyoko katika ala za matamshi za mzungumzaji.
2 x 1

Jina _____ Nambari _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011
SAA: 2 ½

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 3
SAA: 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kijitabu hiki kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

SWALI LA LAZIMA
FASIHI SIMULIZI

1. (a) Tambua tamathali zilizotumika katika methali zifuatazo: (alama5)
   (i) Ujana ni moshi ukienda haurudi.
   (ii) Kupotea njia ndiko kujua njia.
   (iii) Bandubandu humaliza gogo.
   (iv) Usipoziba ufa, utajenga ukuta.
   (v) Chururuu si ndo ndo ndo.

   (b) Nyimbo zina umuhimu gani katika jamii. (alama5)

   (c) Eleza aina zifuatazo za ngano. (alama 5)
   (i) Khurafa
   (ii) Ngano za mashujaa
   (iii) Hekaya
   (iv) Ngano za mtanziko
   (v) Ngano za usuli

   (d) Eleza sifa za ngomezi. (alama 5)

SEHEMU B: TAMTHILIA – KIFO KISIMANI
Kithaka wa Mberia

2. Jibu swali la 2 au la 3
   'Nimeshakwambia tulale hapa langoni! Tulale umati unaokuja kumtoa mfungwa gerezani utukute hapa. Watu wanatupenda sana kwa kazi ya kumzuia mfungwa gerezani. Kwa hivyo tuwasubiri waje watupake mafuta."

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (b) (i) Taja mbinu iliyotumika kwenye dondoo. (alama 2)
   (ii) Fafanua matumizi ya mbinu hii kwenye dondoo. (alama 6)

   (c) Ni maovu gani yaliyotekelezwa na wahusika katika dondoo hii. (alama 8)

3. Jadili huku ukitoa mifano mwafaka matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia kwenye tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20)

SEHEMU C : RIWAYA
UTENGANO : S.A MOHAMMED
Jibu swali la 4 au la 5.

4. Riwaya ya Utengano imejaa kinaya. Fafanua kwa kutoa mifano mwafaka kwenye riwaya. (alama 20)

5. "Now, now, now – tusije huko tena, usinitie kwenye – ee, no"
   (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Taja mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika muktadha huu. (alama 4)
   (c) Mzungumzaji alikuwa amealikwa kwa madhumuni gani? (alama 4)
   (d) Mzungumziwa alipewa mashauri mengi. Yataje. (alama 8)

SEHEMU D : HADITHI FUPI – MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE K.W WAMITILA

6. Zena ni kielelezo cha mwanamke wa kisasa ambaye anajaribu kujikomboa.
Eleza changamoto anazokumbana nazo katika juhudi za kujikomboa. (alama 20)

7. SEHEMU E : USHAIRI

Soma shairi kisha ujibu maswali;

Vile walalama, kwa yale ulotendwa,
Huyakumbuki ya nyuma, pindi ulipochachwa,
Ulipotenda unyama, uliona ndio sawa
Mtenda akitendwa, hulalama kaonewa.

Ulizusha uhasma, leo wewe wapagawa,
Walia bila kukoma, tungedhani umefiwa,
Sasa huna usalama, huwezi kujiopowa!
Mtenda akitendwa, hulalama kaonewa.

Tenda mambo kwa kupima, usiinuke huna bwawa,
Una macho kutazama, na akili umepewa,
Matendo hurudi nyuma, atendaye hurudiwa,
Mtenda akitendwa, hulalama kaonewa.

Dunia haishi njama, sijione umepewa,
Ukadhani u salama, binadamu kupagawa,
Ukahisi ni wanyama, waso hali kama ngawa,
Mtenda alitendwa, hulalama kaonewa.

Unapotenda zahama, siku yako ikakuwa,
Ambapo utaungwama, useme umechachiwa,
Na uanze kutetema, ulie umeonewa,
Mtenda akitendwa, hulalama kaonewa.

Maswali.
(a) Lipe kichwa shairi hili. (alama 2)
(b) Hili ni shairi la aina gani. (alama 2)
(c) Eleza muundo wa ubeti wa pili. (alama 4)
(d) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)
(e) Toa mifano miwili ya inkisari na uindeleze inavyofaa. (alama 4)
(f) Ni kaida zipi zilizotumiwa na mwandishi wa shairi hili. (alama 2)
(g) Eleza maana ya (alama 2)
(i) Uhasama
(ii) Umepowa

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AGOSTI 2011

MJARABU WA KIDATO CHA NNE MUHULA WA PILI 2011 WILAYA YA MASAKU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. (a) (i) Istiara
(ii) Kweli kinzani / paradoski
(iii) Takriri / uradidi
(iv) Chuku
(v) Tanakali za sauti 5 x 1 = 5

(b) - Kuhamasisha watu kufanya jambo
- Kuelimisha jamii.
- Kuhifadhi utamaduni na historia.
- Huburudisha.
- Husifu viongozi.
- Huzindua.
- Kuliwaza / kufariji.
- Njia ya kujipatia riziki.
- Huonya.
- Huhimiza. Zozote 5 x 1 = 5

(c) (i) Ngano ambazo wahusika ni wanyama.
(ii) Ngano ambazo huzungumzia juu ya watu waliotenda matendo ya kishujaa.
(iii) Ngano ambazo mhusika mmoja ni mjanja.
(iv) Ngano ambapo mhusika hujipata katika hali ambapo huhitajika kufanya uamuzi mgumu.
(v) Hueleza asili / chanzo cha kitu, jambo, tabia, maumbile hali n.k
5 x 1 = 5

(d) - Fasihi ya ngoma
- Huwasilisha ujumbe kwa njia fiche inayoeleweka na jamii husika peke yake.
- Ngoma ni muhimu katika kupitisha ujumbe.
- Ujumbe wake hueleweka na jamii husika kwa wepesi.
- Huwasilisha ujumbe wa dharura
- Hudumisha utamaduni wa jamii husika.
- Hutegemea uwezo wa neno sio wa sauti.
- Mapigo yana maana maalumu.
Zozote 5 x 1 = 5

2. (a) Msemaji ni askari II
Anazungumza na askari III
Nje ya gereza
Alikuwa amegundua kuwa Mwelusi alikuwa amekata pingu na umati ulikuwa unawajia
4 x 1 = 4

(b) (i) Kinaya 2 x 1 = 2

(ii) - Watu waliwapenda ilhali waliwachukia.
- Alidai walifanya kazi vizuri ya kumzuia mfungwa lakini wamtesa.
- Alisema watapakwa mafuta, lakini watapigwa.
- Alitaka walale lakini wangekimbia.

Zozote 3 x 2 = 6

(c) - Kuya watu.
- Kula chakula cha mfungwa.
- Kukosea watu adhabu hasa wanawake.
- Kupiga wafungwa.
- Kutusi watu.
- Kutoruhusu wafungwa kuonekana.
- Kukoseana heshima wao kwa wao.
- Kulewa wakiwa kazini.
- Kutolinda raia.
- Kuzika mauti. Zozote 8 x 1 = 8

3. - Mawazo ya Mwelusi yanadhihirika kupitia kwa sauti.
- Bokono kujisemea akikariri maneno ya mpinzani wake.
- Mwelusi akiwa gerezani anajizungumzia awaza jinsi akili ya binadamu hufanya kazi vizuri anapokuwa peke yake.
- Gege anasifu umahiri wake wa ngoma anapoandaa ala yake tayari kwa burudani.
- Tanya anapofurahia kutoroka kwa Mwelusi.
- Bokono anapowaza kuhusu utawala wake kwamba Mungu ndiye aliyempa mamlaka.

Kutaja tukio = 1
Mahali = 1
Mhusika = 1
Sababu ya = 1
Kuzungumza 4 x 5 = 20

4. - Maimuna kutoroka nyumbani akitarajia uhuru na raha badala yake alipata dhiki.
- Maksuudi kujifanya kuwa mcha Mungu na kufanya kinyume kwa kuwa msherati.
- Musa kutembelea mama mzee ni kinaya.
- Maksuudi kuwa tajiri na familia yake kukosa raha.
- Tamima kupata mtoto salama na Maksuudi kumpiga na kumpa talaka badala ya kufurahi.
- Maksuudi kwenda kumwokoa bintiye na kupigwa na umati wa watu.
- Kazija kujirembesha kuwakaribisha wanaume lakini anawachukia.
- Ni kinaya Maimuna kuolewa na Kabi mjukuu wa Farashuu ilhali Farashuu anaichukia familia ya Maksuudi.
- Tamima kuwa mtiifu na mnyenyekevu lakini mumewe anamtawisha na kumpiga.

Zozote 10 x 2 = 20

5. (a) - Msemaji ni Fadhili
- Mzungumziwa ni Maksuudi.
- Nyumbani kwa Maksuudi.
- Fadhili alikuwa amealikwa na Maksuudi ili amsaidie kuepuka kesi ya ufisadi.

4 x 1= 4

(b) - Kuchanganya ndimi
- Mdokezo 2 x 1 = 2

(c) - Maksuudi alitaka Fadhili amsaidie katika kuficha uovu wake.
- Maksuudi alikuwa fisadi, mtuhumiwa na hakutaka sifa yake mbaya ijulikane na wapiga kura.

2 x 1 = 2

(d) - Alimweleza kuwa alikuwa mtumishi wa umma na hakuwa tayari kujiharibia sifa.
- Alikataa kuididimiza kesi.
- Enzi ya ukoloni imepita.
- Alikuwa amemwonya mara nyingi lakini alikuwa amesahau.
- Alimwonya dhidi ya ufisadi.
- Alimfahamisha kuwa wananchi ni wa maana kuliko viongozi.
- Wananchi wamechoka na viongozi wabinafsi.
- Fadhili hangeweza kununuliwa na pesa.

Zozote 8 x 1 = 8

6. - Ubaguzi wa kijinsia – Mwanamke kubaguliwa kielimu.
- Ndoa za mapema.
- Ndoa za lazima.
- Kuchaguliwa wachumba.
- Mtatizo ya unyumba – kutusiwa, dharauliwa kuwekwa kama vyombo vya burudani vya wanaume
- Ubaguzi wa kisiasa – kutopewa nafasi ya kuingia kwenye siasa
- Kunyimwa uhuru wa kufanya maamuzi yanayowahusu.
- Umaskini – Zena alikosa pesa za kufanya kampeni.

Mfano 1
Maelezo 3
4 x 5 = 30

7. (a) Mtenda akitendwa 2 x 1 = 2

(b) Tarbia – Mishororo minne katika kila ubeti 2 x 1 = 2

(c) - Mishororo minne
- Vipande viwili
- Mizani nane – Ukwapi na utao
- Mpangilio wa vina
  - Ma – wa
  - Ma – wa
  - Ma – wa
  - Wa – ma

4 x 1 = 4

(d) Ni vipi unakasirika kwa yale uliyotendewa hukumbuki yaliyopita baada ya kukasirika wewe
- Ulipotenda mabaya hukujali.
- Mtu anayetenda mabaya hulalamika.

4 x 1 = 4

(e) Ulotendwa – Uliotendwa
Kaonewa – Ukaonewa
Sijione – Usijione
Waso – Wasio

Zozote 2 x 1 = 2

(f) - Urari wa vina
- Urari wa mizani
- Mishororo
- Beti
- Muwala
- Vipande
- Kibwagizo

Zozote 4 x 1 = 4

(g) (i) Chuki
(ii) Umetulia, umenyamaa / umenyamaza

Zozote 2 x 1 = 2